

## **CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA KIBABII**

**(CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
CHA MASINDE MULIRO)**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRINKA**

**KIS 211: ORAL LITERATURE IN KISWAHILI (FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI)**

### **UTANGULIZI**

Kozi hii inalenga kumtanguliza mwanafunzi kuhusu fasihi simulizi kama aina ya fasihi. Kozi hii inafafanua dhana ya fasihi simulizi, sifa za fasihi simulizi, uainisishaji wa fasihi simulizi, nadharia katika fasihi simulizi na kushughulikia utafiti katika fasihi simulizi

### **MADHUMUNI YA KOZI**

Kufikia mwisho wa kozi hii, mwanafunzi aweze:

Kueleza maana ya fasihi simulizi na kujadili umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii

Kujadili sifa bainifu za fasihi simulizi; kufafanua tanzu za fasihi simulizi

Kueleza mabadiliko katika fasihi simulizi

Kuzingatia nadharia katika utafiti wa fasihi simulizi;

Kukusanya, kurekodi na kuhifadhi data kama hatua muhimu ya nyanjani katika fasihi simulizi

### **MATOKEO YA UJIFUNZAJI**

Inatarajiwu kuwa, baada ya kozi hii mwanafunzi ataweza kutekeleza mambo yafuatayo:

Kueleza maana na fasihi simulizi na kujadili umuhimu wake katika jamii

Kujadili sifa bainifu za fasihi simulizi; kufafanua tanzu za fasihi simulizi

Kueleza mabadiliko katika fasihi simulizi

Kuzingatia nadharia katika utafiti wa fasihi simulizi na kutumia hatua za nyanjani katika kuimarisha fasihi simulizi

## **YALIYOMO**

Maana ya fasihi simulizi, sifa za fasihi simulizi, Dhima ya fasihi simulizi, Tofauti na mfanano wa fasihi simulizi na fasihi andishi,

Tanzu za fasihi simulizi- vigezo vya muainisho,

Nadharia katika fasihi simulizi: Ueneaji, Mabadiliko, Udenguzi, Umuundo

Mbinu za utafiti katika fasihi simulizi; Matatizo ya mbinu za utafiti katika fasihi simulizi; Matatizo ya nadharia za utafiti katika fasihi simulizi; Ukusanyaji wa data katika fasihi simulizi; Uhifadhi wa data katika fasihi simulizi;

Uchanganuzi wa data katika fasihi simulizi; Matumizi ya data katika fasihi simulizi;

Mielekeo kuhusiana na fasihi simulizi;

Umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii.

## **UFUNDISHAJI / UTATHMINI WA KOZI**

Mwanafunzi atawajibika kuhudhiria mihadhara yote. Mbali na mahudhurio ya mihadhara, atafanya mijarabu miwili ambayo itachangia asilimia thelathini ya jumla ya tuzo katika muhula. Mwishowe mwanafunzi atafanya mtihani ambao utachangia asilimia sabini ya alama za muhula.

## **MAREJELEO**

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Kitula, K. na Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: KLB

Miruka, O. (1994). *Encounter with Oral Literature*. E. A. E. P.

Miruka, O. (1999). *Studying Oral Literature*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers

Ngaruthi K. (2007). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundations.

P'Bitek, O. ( 1986). *Artist the Ruler*. Nairobi: E.A.E. P.

Wamitilla, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi*. Nairobi: Focus Publication Limited.

Tanbihi: Marejeleo zaidi yatatolewa darasani.

**Mhadhiri: Bi. Muindu K. Gladys – 0721895156**